**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**

**03** **MAARIFA YA JAMII**

**Muda: Saa 1:30** **MAJIBU** **Mwaka: 2021**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali manne (4).
2. Jibu maswali yote katika kila sehemu.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

***Prepared by Maria Marco for TETEA***

SEHEMU A (Alama 28)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Jibu kipengele cha (i) – (viii) kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuiandika katika kisanduku.

(i) Kipi kinahusika zaidi na uharibifu wa mazingira katika maeneo ya vijijini?

A. Kelele kutoka gereji na karakana

B. Moshi wa viwandani

C. Hewa chafu kutoka katika magari na mashine

D. Uchomaji wa mkaa

**D. Uchomaji wa mkaa**

Uchomaji wa mkaa hutokea zaidi vijijini na husababisha ukataji wa miti ovyo, hivyo kuharibu mazingira.

(ii) Vipi miongoni mwa vitu vifuatavyo vinawakilisha sehemu ya mazingira ya mjini?

A. Mapori, mashamba na wanyama

B. Maduka makubwa, viwanja vya ndege na hospitali

C. Mashamba makubwa, mapori na wanyama

D. Mapori, mashamba na maduka

**B. Maduka makubwa, viwanja vya ndege na hospitali**

Hivi ni vipengele vinavyopatikana zaidi katika mazingira ya mjini.

(iii) Yapi ni matumizi ya mbao?

A. Kuchoma mkaa

B. Kutengeneza kamba

C. Kutengeneza samani

D. Kutengeneza magari

**C. Kutengeneza samani**

Mbao hutumika sana kutengeneza samani kama meza, viti na makabati.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

***Prepared by Maria Marco for TETEA***

(iv) Hewa inayosafiri hujulikana kama:

A. Upepo

B. Maji

C. Jotoridi

D. Mawingu

**A. Upepo**

Hewa inayotembea kutoka sehemu moja kwenda nyingine huitwa upepo.

(v) Mazingira yamegawanyika katika makundi makuu mawili ambayo ni:

A. Vitu hai na mimea

B. Vitu visivyo hai na wanyama

C. Vitu hai na visivyo hai

D. Mimea na wanyama

**C. Vitu hai na visivyo hai**

Mazingira hujumuisha viumbe hai na vitu visivyo na uhai.

(vi) Ipi ni kazi kubwa ya majumba ya makumbusho?

A. Kuhifadhi wageni kutoka nje ya nchi

B. Kutangaza taarifa za kihistoria

C. Kuhifadhi kumbukumbu za kihistoria

D. Kuhifadhi mapambo

**C. Kuhifadhi kumbukumbu za kihistoria**

Makumbusho hulinda na kuhifadhi historia na urithi wa taifa.



Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

***Prepared by Maria Marco for TETEA***

(vii) Kwanini mazingira machafu ni mabaya kwa afya?

A. Husababisha ulemavu

B. Husababisha uzembe

C. Husababisha umaskini

D. Husababisha magonjwa

**D. Husababisha magonjwa**

Mazingira machafu huzalisha vijidudu vinavyosababisha magonjwa.

(viii) Kazi ipi ya binadamu husababisha uchafuzi wa hewa?

A. Viwanda

B. Utalii

C. Biashara

D. Uvuvi

**A. Viwanda**

Viwanda huzalisha moshi na gesi chafu zinazochafua hewa.

2. Oanisha changamoto za shughuli za kiuchumi zilizopo katika Fungu A na aina ya shughuli za kiuchumi katika Fungu B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

(i) Kukosekana kwa malisho mazuri

**E. Ufugaji wa wanyama**

(ii) Kupungua kwa samaki kutokana na matumizi ya sumu na nyavu zenye matundu madogo

**G. Uvuvi**

(iii) Kukosekana kwa teknolojia ya kisasa katika migodi

**C. Uchimbaji wa madini**


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

***Prepared by Maria Marco for TETEA***

(iv) Matangazo duni ya kuvutia wageni kuja kuangalia urithi wa asili na mbuga za wanyama

**F. Utalii**

(v) Utengenezaji wa mkaa na kukata miti ovyo

**B. Misitu**

(vi) Kupungua kwa chakula kutokana na upungufu wa mvua na udongo kukosa rutuba

**A. Kilimo**

SEHEMU B (Alama 22)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

3. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

Ujima ulikuwa mfumo wa kwanza wa kiuchumi ambao binadamu wote waliupitia. Hapakuwa na unyonyaji miongoni mwa watu kwa kuwa kila mmoja alishiriki katika uzalishaji. Katika mfumo huu, njia kuu za uzalishaji mali zilikuwa ardhi, misitu, maziwa na mito. Wakati wa ujima, uzalshaji mali ulikuwa mdogo sana. Hii ilitokana na vitendea kazi duni vilivyotumika.

Vilevile hapakuwa na biashara wala kubadilishana bidhaa baina ya watu katika jamii. Hii ilitokana na kukosekana kwa ziada wakati wa kuzalisha. Mfano wa vitendea kazi vilivyotumika ni majembe ya mkono na mishale. Katika kipindi cha ujima, njia za uzalishaji mali na vitendea kazi vilimilikiwa na jamii nzima.

**Maswali:**

(i) Bainisha njia mojawapo kuu ya uzalishaji mali wakati wa ujima.

Njia mojawapo kuu ilikuwa ardhi.

(ii) Kifaa gani kilitumika katika kuwinda?

Kifaa kilichotumika ni mishale.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

***Prepared by Maria Marco for TETEA***

(iii) Kwa nini hapakuwa na unyonyaji katika mfumo huu wa uzalishaji mali?

Hapakuwa na unyonyaji kwa sababu kila mtu alishiriki katika uzalishaji mali kwa usawa.

(iv) Kwanini hapakuwa na biashara katika mfumo huu wa uzalishaji mali?

Hapakuwa na biashara kwa sababu hakukuwa na ziada ya mazao ya kubadilishana.

(v) Nani alifaidika kutokana na mali zilizozalishwa katika mfumo huu wa uzalishaji mali?

Waliofaidika ni jamii nzima.

(vi) Kwanini hapakuwa na mazao ya ziada yaliyozalishwa katika mfumo huu wa uzalishaji mali?

Kwa sababu vitendea kazi vilivyotumika vilikuwa duni hivyo uzalishaji ulikuwa mdogo.

(vii) Ni kwa jinsi gani njia za uzalishaji mali zilimilikiwa?

Njia za uzalishaji mali zilimilikiwa kwa pamoja na jamii nzima.

4. Soma ramani ya Kijiji cha Lumbila kisha jibu kipengele cha (i) – (iv) kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

    (i) Kuna shule ngapi katika kijiji cha Lumbila? **Shule mbili**

    (ii) Kanisa lipo upande gani toka daraja lililo karibu? **Kusini**

    (iii) Kuna milima mingapi katika kijiji cha Lumbila? **Mitatu**

    (iv) Ni barabara ngapi zinaelekea Kaskazini mwa Kijiji cha Lumbila? **moja**


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

***Prepared by Maria Marco for TETEA***